Maswali na Majibu kuhusu watoto walio zeruzeru.

Kuletwa kwenu na Every Child Ministries
Shirika lisilo la serikali la kikristo liletayo tumaini kwa “watoto waliosahaulika wa Afrika”.
Kwa maana WATOTO ni rasilmali kubwa kwa nchi yeyote –
Tunu kutoka kwa Mungu!

Uzeruzeru ni nini?
Uzeruzeru ni seti au jozi za maumbile za maumbile zilizorithiwa. Haya maumbile yaletwa na ukosefu wa rangi aina ya “melanini” kwenye ngozi , macho na nywele, na hufanya ngozi zao na macho yawe na uroro kutokana na mwangaza na uonaji hafifu.

Je, uzeruzeru ni ugonjwa?
La, siyo ugonjwa na hausababishwi au kusambazwa na viini au virusi. Mtoto siyo mgonjwa na hakuupata uzeruzeru kama mtu apatavyo ugonjwa wakuenezwa ila hawezi kusamabaza hali hii kutokana na mawasiliano. Kwa hivyo, ni sawa kumgusa zeruzeru kama umgusavyo mtu mwingine.

Ni salama kununua chakula kutoka kwa zeruzeru au kula chakula kilichotayarishwa naye?
Ndiyo kabisa. Uzeruzeru siyo ugonjwa. Hakuna viini au virusi vya aina yoyote vinavyo husiana na uzeruzeru.

Je, uzeruzeru ni laana?
La, siyo laana. Bibilia yasema kuwa watoto wote ni baraka kutoka kwa Mungu na zawadi kwa jamii. Mtoto zeruzeru anaweza kukua kawaida na kuleta baraka tele kwenye jamii, jamaa na ulimwengu wote.

Yaleta laana kwa mwanamke mjamzito kumwangalia zeruzeru?
La, kumwangalia mtu hakuwezi kudhuru mimba yake.

Ni aibu kuwa na mtoto zeruzeru?
La, mtoto zeruzeru ni tofauti na mwingine lakini kumzaa zeruzeru si aibu kwa mzazi. Mtoto ni baraka tele wakati wote.

Je, zeruzeru ana nguvu spesheli au vipawa vya ajabu?
La, zeruzeru ni watu kama wengine.Kufanya mapenzi na zeruzeru hakuponyi ugonjwa wowote. Viungo vya mwili vya zeruzeru havina vipawa au nguvu spesheli .Wachawi wanapenda kutengeneza pesa kwa kudanganya uma na uongo huu. Mnamo mwaka wa 2007 wachawi wa kutoka Tanzania waligundua wangeweza kutengeneza pesa kutokana na uongo huu. Hii ilisababisha mauwaji yamazeruzeru wengi , lakini hakuna hata mtu mmoja aliyeponywa.
Huko Zimbabwe wengine wafikiri kufanya mapenzi na zeruzeru kutaponya Ukimwi. Lakini hakuna ukweli wowote kutokana na imani hii. Wanawake zeruzeru hutaabika sana kwa kubakwa na kusambaziwa ukimwi na wanaume hawa.

Je, mazeruzeru wako na akili punguani?
La, mazeruzeru hawana ulemavu wa akili. Wana akili sawa kama watoto wengine na wanaweza kuwa werevu sana. Kama ni walegevu inapasa wazazi waangalie kama wana shida za macho. Yawezekana kwamba hawawezi kuona ubao mweusi darasani, au kuona ili wasome vyema.,kwa hivyo kudhuru masomo yao. Mara kwa mara, watoto zeruzeru hupata shida za kutofautisha. Hii inaweza kudhuru uwezo wao wa kusoma na kufanya hesabu, wakipata usaidizi mazeruzeru waweza kufaulu kwa somo lolote kama watoto wengine.

Kama haya mashauri hayataweza kusaidia uonaji wa zeruzeru, atafanya nini?
Anaweza kuangaliwa na daktari wa macho. Mara kwa mara, miwani zaweza kusaidia,lakini si miwani zozote. Ni lazima apimwe mwenyewe. Zeruzeru wengine wanaweza kutumia glasi za kusoma za kushikilia. Baadhi ya

mazeruzeru ni vipofu au hawaoni vizuri. Wanaweza kujifunza maandishi ya vipofu na kuishi kama vipofu. Kwa watu walio na uzeruzeru, kuongeza ukubwa wa kitu hakutamsaidia daima akione vyema
Kuongeza ukubwa wa maandishi mara kwa mara husaidia haswa- kwa mfano kutumia kalamu nyeusi kwa karatasi nyeupe, ama kutumia ubao mweusi sana badala ya ubao wa rangi ya kijani.

Je, zeruzeru anahitaji kutengezewa miwani spesheli za kukinga jua?
Miwani za kukinga jua huwasadia mazeruzeru kukinga macho dhidi ya miale haribifu ya jua. Walakini, hazi imarishi kuona, ila ni muhimu kusaidia macho yasizidi kuhadhirika na jua kali. Pia huwapatia tulizo, kwani jua kali huumiza macho ya zeruzeru mno.

Zeruzeru anaweza kuishi kwa mda gani?
Zeruzeru anaweza kuishi kwa mda wa kawaida, ilimradi asipate saratani kwa kutokinga ngozi yake dhidi ya miale ya jua. Kuna aina moja hasa ya zeruzeru itwayo 'Hermansky – Pudlak syndrome' ambayo huambatana na utokaji wa damu na yaweza kudhuru mapafu na matumbo, kwa hivyo kufupisha mda wa kuishi. Wengi wa mazeruzeru waweza kuwa na mda wa kuishi wa kawaida . Kuwa zeruzeru hakusababishi kifo.

Je, mazeruzeru wanaweza kuolewa na kupata watoto?
Ndio, mazerzeru wako kamili kimwili. Wana uwezo wa kuzaa na pia kuweza kujali nyumba zao na familia. Wanahutaji tu kinga hususan dhidi ya jua.

Hali ya baadaye ya mazeruzeru ni ipi? Waweza kuishi maisha gani?
Mazeruzeru wamepata fanaka katika nyanja nyingi maishani. Mfalme mmoja wa japani alikuwa zeruzeru. Baadhi ya waigizaji, wanavichekesho, wanamuziki maarufu ni mazeruzeru, pia warembo wa fesheni , wanabiashara za kimataifa, wakufunzi na wengineo.
Umaarufu wao unategemea mwongozo wao binafsi na msaada au auni kutoka kwa familia na jamii.
Kwa sababu ya uroro kutokana na jua, ni bora watoto zeruzeru wafanye kazi zao ndani.

Ni nani anadhurika sana, wavulana au wasichana?
Madhara ni sawa kwa wote.

Je, uzeruzeru wapatikana bara la Afrika tu?
Uzeruzeru wapatikana kote ulimwenguni,lakini zaidi katika bara la Afrika, haswa kwenye watu wa rangi nyeusi. Hata wanyama waweza kuwa zeruzeru.

Wazazi wakipata mtoto moja zeruzeru, Je, watoto wote watakuwa zeruzeru?
Sio hasa, kama wazazi wamepeba jozi ya uzeruzeru, kuna uwzekano wa asilimia robo kuwa mtoto atakuwa zeruzeru.

Je, Mungu awajali zeruzeru?
Mungu awajali viumbe vyote. Bibilia yasema kuwa hakuna ndege wa angani ataanguka bila Mungu kujua. Yesu alisema kwamba hata maua uwanjani yako kwa mikono ya (Mathayo 6:26 na 28). Mungu awapenda watu wote hata kama wana ulemavu wowote, hachagui, " Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu, hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ilakila amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16)".

Every Child Ministries Uganda
PO Box 28080 Kampala
ecmuganda@yahoo.com
www.ecmafrica.org